بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وعد الله الذين آمنوا منكم وعملوا الصالحات ليستخلفنهم في الأرض كما استخلف الذين من قبلهم وليمكنن لهم دينهم الذي ارتضى لهم وليبدلنهم من بعد خوفهم أمنا يعبدونني لا يشركون بي شيئا ومن كفر بعد ذلك فأولئك هم الفاسقون﴾

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

**Toleo: 1445/02 H** | **Alhamisi, 23 Muharram 1445 H** | **10/08/2023 M**


**<u>Taarifa kwa Vyombo vya Habari</u>**

# Ujumbe kutoka Hizb ut Tahrir / Kenya Ulikutana na Sheikh Abdul Halim Hussain, Kadhi Mkuu wa Kenya

**(Imetafsiriwa)**

Ujumbe kutoka Hizb ut Tahrir / Kenya, ukiongozwa na Ustadh Mahd Ali, mkuu wa Kamati Kuu ya Mawasiliano ya Hizb ut Tahrir Kenya, akiandamana na Ustadh Shaaban Mwalimu, mwakilishi kwa vyombo vya habari wa Hizb ut Tahrir Kenya, na Ustadh Shaaban Rajab, mwanachama wa Kamati Kuu ya Mawasiliano ya Hizb ut Tahir Kenya, walikutana na **Sheikh Abdul Halim Hussain,** Kadhi Mkuu wa Kenya anayeishi jijini Nairobi.

Ujumbe wa Hizb ulipokewa kwa uchangamfu, na mkuu wa ujumbe huo, Ustadh Mahd Ali, na Ustadh Shaaban walimpongeza kadhi huyo na kumshauri juu ya umuhimu wa kushikamana na Uislamu katika nyanja zote za maisha. Walimpa vitabu viwili, *Njia (Manhaj) ya Hizb ut Tahrir ya Mageuzi* na *Al-Khilafah*.

Ujumbe huo pia ulikutana na **Sheikh Mohammed Uthman, Imamu wa Msikiti wa Landis jijini Nairobi.**

Twamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu afungue nyoyo za Ulema (wanazuoni) kufanya kazi na Hizb ut Tahrir katika kuregesha mfumo kamili wa maisha ya Kiislamu kupitia kusimamisha Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Kenya**


**Simu**: +254 707458907
**Pepe:** mediarep@hizb.or.ke
**Tovuti ya Hizb ut Tahrir Kenya:** www.hizb.or.ke

**Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:** www.hizb-ut-tahrir.org
**Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:** www.hizb-ut-tahrir.info